



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Kwanza

IBRAHIMU AFUATA UONGOZI WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 11:27-12:9; Waebrania 11:8-10

Miaka mingi sana baada ya gharika kuu ya siku za Nuhu, kulikuwa na mtu mmoja aliyetwa Abram. Alikuwa uzao wa Shemu, mmojawapo wa wana wa Nuhu. Jamaa ya Nuhu walitawanyika chini na walikaa katika mahali pengi. Abram alikaa na Tera, baba yake, katika mji wa Uru katika nchi ya Wakaldayo. Lutu, mwana wa nduguye Abram, pia alikaa na Tera.

Wakazi wa Uru hawakumwabudu Mungu, bali waliabudu sanamu. Walikwisha kumsahau Mungu tangu wakati wa Nuhu. Jambo hili linaonekana kuwa ajabu, lakini watu hawa walimwacha Mungu hata baada ya Mungu kuiharibu nchi kwa gharika. Lakini Abram alimkumbuka Mungu. Mungu aliona kwamba Abram alikuwa mtu ambaye angefanya mambo aliyotaka. Sarai, mkewe Abram, pia alimwabudu Mungu na hakuabudu sanamu za majirani zao.

Abram alikuwa mzee wakati Mungu alipomwita kuondoka Uru. Mungu alimwambia, "Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha." (Mwanzo 12:1) Abram alikuwa tayari kuondoka kwenda kama Bwana alivyomwambia, lakini hakujua nchi iliyompasa kwenda. "Kwa imani Abram alipoitwa aliitika...akatoka asijue aendako." (Waebrania 11:8)



Abramu pamoja na jamaa yake yote waliondoka Uru, wakaanza kusafiri kwenda katika nchi ambayo Mungu angemwonyesha. Alimchukua Sarai mkewe, Lutu mwana wa nduguye, Tera baba yake, kondoo, mbuzi, na ng'ombe zote. Safari yao iliwaongoza kupitia jangwani na mtoni ambako hakukuwa na watu, lakini Abramu hakuogopa kwa sababu alimwamini Mungu.



Wakati Abramu alipofika Harani, alikaa hapo kwa miaka michache. Baba yake alikufa, kisha Mungu alimwambia kuendelea na safari. Safari ya kwenda kwa nchi mpya ilichukua miaka mitano. Wakati Abramu na jamaa yake walipofika Shekemu, Mungu alimwambia ya kwamba sasa alikuwa katika nchi aliyomtaka kuitwaa.

Abramu alijenga madhabahu ya kumwabudia Mungu na kumshukuru. Pia, alijenga madhabahu Betheli. Mungu aliahidi kumfanya kuwa baba wa mataifa mengi. Hakuwa na watoto, lakini aliamini ya kwamba mambo Mungu aliyoyasema yangefanyika.



Siku moja usiku Mungu alimwambia Abramu kutoka nje kutazama nyota na kuzihesabu. Abramu hakuweza kuzihesabu. Basi, Mungu alimwambia kwamba uzao wake ungekuwa mwingi kama nyota. Alimwamini Mungu.

Abramu alipokuwa na umri karibu miaka mia moja, Mungu alimkumbusha tena ahadi ile. Mungu alimwambia ya kwamba Sarai mkewe angemzalia mtoto mwanamume, na mtoto huyu wangemwita Isaka. Jamaa yake ndio wangukuwa mwanzo wa mataifa mengi ambayo yangufuata. (Tazama Mwanzo 17.) Abramu aliitwa Ibrahimu kwa sababu angekuwa baba wa mataifa mengi.

KAZI YA KUFANYA:

Chora mstari kutoka kwa sehemu ya kwanza ya sentensi hadi kwa sehemu ya pili inayoikamilisha vyema.

1. Tera alikuwa mji ambao Abramu alikaa kwanza.
2. Uru ulikuwa mwana wa nduguye Abramu.
3. Lutu alikuwa mkewe Abramu.
4. Sarai alikuwa babaye Abramu.

Soma Waebrania 11:8-10 ukamilishe sentensi zifuatazo hapo chini:

1. Abramu alimtii Mungu kwa sababu alikuwa na _____.
2. Wakati Ibrahimu aliposafiri, alikaa katika _____.

Chagua jibu lililo kweli ucho-re
mvingo kwa herufi iliyo kando yake.

**1. Ibrahimu hakuogopa wakati
aliposafiri kwa sababu...**

- a. Alimwamini Mungu.
- b. Alikuwa na jamaa wengi
pamoja naye.

c. Lutu aliahidi kumlinda.

**2. Wakati Ibrahimu alipofika katika
Nchi ya Ahadi...**

- a. Alikaa Yerusalemu.
- b. Alijenga madhabahu.
- c. Alinung'unika kwa sababu
hapakuwa na miji.

**3. Mungu alisema ya kwamba uzao
wa Ibrahimu ungekuwa mwingi
usioweza kuhesabiwa kama...**


- a. Kundi la mifugo.
- b. Mawingu mbinguni.
- c. Nyota.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

**"Kwa imani Ibrahimu alipoitwa
aliitika, atoke aende mahali pale
atakapopapata kuwa urithi; akatoka
asijue aendako." Waebrania 11:8**

Wakati Mungu alipomwambia,
Abramu kuondoka kwao, Abram^u
aliondoka, akaenda. Hakujua mahali
Mungu alikomtaka kwenda, lakini
alikuwa kufanya jambo Mungu
alilotaka. Abram^u alijua kwamba
mpango wa Mungu kwake ulikuwa
mzuri kwa hivyo hakuogopa.

Je! tunakubali kutenda mambo
ambayo Mungu anatuuliza? Ndiyo.
Mungu anataka tupende majirani zetu.
Anataka twende kanisani kujifunza
Biblia aliyotupa. Tunajua ya kwamba
mpango wa Mungu ni mzuri, kwa hivyo
tunakubali kufanya kama anavyo-
tuuliza.





VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Pili

WAJUKUU WA IBRAHIMU

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 25:19-34; Mwanzo 27:1-46

Isaka alizaliwa wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka mia moja. Angekuwa kiongozi wa mataifa mengi. Lakini Mungu alimjaribu Ibrahimu wakati Isaka alipokuwa mdogo kuona kama angeendelea kuwa mwaminifu kwake.



Mungu alimwambia Ibrahimu kumtoa Isaka kama sadaka ya kuteketezwa. Ibrahimu hakufahamu kwa nini Mungu wa kweli alimtaka kufanya jambo kama hilo, lakini alimwamini. Mungu hakumruhusu Ibrahimu kumdhuru Isaka wakati alipoiona imani ya Ibrahimu.

Wakati Isaka alipotimiza umri wa miaka arobaini, Ibrahimu aliwatuma watumishi wake kwenda kumtafutia mke. Walikwenda kama walivyo-ongozwa na Mungu mpaka mji wa Harani. Walimletea Isaka msichana mzuri ambaye aliitwa Rebeka. Wakati Isaka alipokuwa na umri wa miaka sitini, mkewe alimzalia watoto wawili mapacha, Yakobo na Esau.

Yakobo na Esau hawakufanana. Esau alipenda kuwinda na kukaa nyikani. Lakini Yakobo alipenda kukaa hemani na hakujali kuwinda. Haiwapasi wazazi kumpenda mtoto mmoja zaidi kuliko mwingine, lakini Isaka alimpenda Esau zaidi. Rebeka alimpenda Yakobo zaidi kuliko Esau.

Jambo hili lilileta shida katika jamaa ile.

Siku moja, wakati Esau alipokwisha kuwinda kwa muda mrefu na kusikia njaa, alikuja nyumbani. Wakati alipokuja, alisikia harufu ya chakula ambacho Yakobo alikuwa akipika.



Alitaka zaidi kupata chakula kile kuliko kitu kingine. Kwa hivyo aliahidi kumwzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza ili angepata chakula kile. Hakuheshimu ahadi ya Mungu, lakini Yakobo alitaka kuwa kiongozi wa taifa ambalo Mungu aliahidi.

Ndugu hawa wawili hawakuishi kwa furaha pamoja baada ya jambo hili. Ilikuwa kosa kwa Esau kutojali haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Lakini ilikuwa kosa pia kwa Yakobo kumdanganya ndugu yake.

Yakobo alimdanganya baba yake pia. Wakati ambapo Esau angepokea baraka za baba yake kama mzaliwa wa kwanza, Yakobo alijivika ngozi mikononi mwake, akachukua mahali pa Esau. Isaka alikuwa mzee sana karibu na kufa hata hakuweza kumtambua Yakobo, kwa hivyo alimpapasa tu mikono kama alikuwa Esau kweli. Aliposikia mikono yake



ikiwa na malaika, alikuwa na hakika kwamba alikuwa akimbariki Esau, mwanawe mkubwa. Yakobo aliiba baraka za Esau kutoka kwa baba yake, lakini Esau alikwisha kukubali kuzipoteza.

Mungu angeendelea kutimiza ahadi na mpango wake kwa Yakobo. Mungu alijua kwamba mambo haya yangetokea, lakini hivyo si kusema kwamba alifikiri ilikuwa haki kudanganya au kuiba. Mungu hakukubali matendo haya.

KAZI YA KUFANYA:

Jibu mwalimu maswali yafuatayo:

1. Je! Mungu alimjaribu Ibrahimu kwa jinsi gani kuona kama alikuwa mwaminifu? _____
2. Isaka alipata mke kwa jinsi gani? _____



Yakobo

Esau

Andika jina la Yakobo au Esau katika mistari iliyo kando ya sentensi zifuatazo kuzikamilisha vyema.

_____alipenda kuwinda na alikaa nyikani.

_____alipenda kukaa hemani.

_____alipendwa zaidi na baba yake.

_____alipendwa zaidi na mama yake.

Jaza vyema nafasi zilizoachwa.

Yakobo aliiba vitu viwili kutoka kwa ndugu yake kwa njia ya udanganyifu. Aliiba _____ ya ndugu yake ya mzaliwa wa kwanza na _____ zake.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Chakula cha mboga penye mapendano; ni bora kuliko ng’ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.”
Mithali 15:17

Yakobo hakutenda mambo mema tu kila siku. Lakini Mungu alimpenda na alitaka kumfanya kuwa kiongozi wa mataifa mengi ambayo Mungu alimwahidi Ibrahimu. Yakobo alisikitika kwa dhambi aliyoitenda na Mungu alimbariki.

Je! wakati mwingine tunatenda mambo mabaya? Ndiyo. Lakini Mungu bado anatupenda. Anataka tuhuzunike kwa ajili ya dhambi zetu ili aweze kutusaidia kujifunza kuwa watu wema.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Tatu

YAKOBO APEWA JINA JIPYA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo
28:10-33:20; Matendo 11:26

Esau alimkasirikia sana Yakobo na alipanga kumwua mara tu baada ya baba yao kufa. Rebeka hakumwambia Isaka ya kwamba vijana wao walikasirikiana. Alisema tu ya kwamba ilimpasa Yakobo kurudi Harani kutafuta mke. Jambo hili lilimpendeza Isaka, kwa hivyo Yakobo aliondoka nyumbani mwao akiwa amebarikiwa na Isaka babaye.

Bila shaka Yakobo alifikiri juu ya ahadi ambayo Mungu alimwahidi Ibrahimu, babu yake, na Isaka, baba yake, na ambayo sasa ilikuwa kwake. Alikuwa na muda wa kufikiri wakati alipokuwa akisafiri kwenda Harani.

Isaka babaye Yakobo alikuwa akikaa Beer-sheba. Safari kutoka Beer-sheba kwenda Harani ilichukua siku nyingi. Yakobo aliondoka kwao, akawaacha baba yake na mama yake na ndugu yake aliyekasirika naye. Labda alifikiri kwamba alimwacha Mungu pia nyuma.



Baada ya kusafiri siku ya kwanza mchana kutwa, Yakobo alisimama mahali kulala. Alichukua jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi. Usiku ule aliota ndoto ya ajabu kwamba ngazi ilikuwa ikisimama juu ya nchi, na ncha yake ilifika mbinguni, na kwamba malaika walikuwa wakipanda na kushuka juu yake. (Tazama Mwanzo 28:12-15.) Mungu alimwahidi Yakobo ahadi ya ajabu wakati ule alipokuwa akilala.



Wakati Yakobo alipoamka, alijua kwamba hakumwacha Mungu nyuma katika mji wao wa Beer-sheba. Alijua kwamba Mungu alikuwapo pamoja naye wakati wote.

Yakobo hakujiona kuwa peke yake tena wakati aliposafiri kwa sababu Mungu alikuwapo pamoja naye. Baada ya kusafiri siku nyingi, alifika karibu na Harani. Katika mahali pale palikuwa na kisima, na Yakobo alimwona Raheli kwanza hapo kisimani. Alimsaidia Raheli kuwanywesha kondoo zake, kisha alimtuma kwenda kumwambia mjomba wake ya kwamba alikuja.



Babaye Raheli alikuwa Labani. Labani alikuwa pia mjomba wa Yakobo. Yakobo alipomwambia Labani kwamba alitaka kumwoa Raheli, Labani alimwambia kumfanyia kazi miaka saba ndipo angempata Raheli. Baada ya arusi, Yakobo alitambua kwamba alimwoa Lea, dada

mkubwa wa Raheli badala ya Raheli. Labani alimdanganya. Ilimbidi kufanya kazi tena miaka mingine saba kumpata Raheli.

Wakati Yakobo alipomfanyia mjomba wake kazi, alilipwa ujira wa mifugo. Baada ya muda mfupi alianza kutajirika kwa sababu Mungu alimbariki. Labani aliona wivu, Yakobo akaona kwamba ilimpasa kuondoka mara moja kwa mjomba wake. Labani hakumtaka Yakobo kuondoka, lakini Yakobo aliona kwamba mjomba wake hakuwa na urafiki naye. Aliondoka pamoja na wanawake zake na mali yake.

Wakati Yakobo alipokaribia Beer-sheba, mjini kwao, alianza kuogopa juu ya hasira ya ndugu yake. Watumishi walikuja kwake wakisema ya kwamba Esau alikuwa akija pamoja na watu mia nne kumlaki. Yakobo aliogopa sana alipofikiria hasira ya ndugu yake.

Malaika wa Mungu alimjia Yakobo, Yakobo akamwambia kwamba hangeondoka mpaka angembariki. Baraka ya Yakobo ilikuwa jina jipya, Israeli, ambalo maana yake ilikuwa "Mwana wa mfalme wa Mungu." Yakobo alijua ya kwamba Mungu alikuwa akimkumbusha juu ya Ahadi yake Kuu. Alimshukuru Mungu na alijua kwamba alikuwa salama. Mungu aliahidi kuanzisha taifa kubwa kwake.

Wakati Yakobo alipokutana na Esau, walifurahi sana kuonana tena, na hawakuwa na ugomvi. Yakobo alikuwa sasa akiitwa Israeli. Alipiga kambi yake karibu na Esau ndugu yake. Katika kila mahali ambapo Israeli alipiga hema alimjengea Mungu madhabahu. Hii ilionyesha kwamba alikuwa na imani



katika Mungu na aliamini kwamba Mungu alikuwapo pamoja naye sikuzote.

KAZI YA KUFANYA:

Chora mistari kutoka kwa sentensi upande wa kulia hadi kwa maneno ya kumalizia upande wa kushoto ambayo ni kweli.

kwenda kutafuta
mke.

Yakobo ali-
ondoka
nyumbani

kumkimbia Esau.
kutatfuta Nchi ya
Ahadi.

Wakati Yakobo alipouliza kumwoa Raheli, Labani babaye Raheli alisema kwamba ilikuwa lazima Yakobo kumfanyia kazi miaka _____ (mingapi?)

Yakobo alipewa jina jipya na

Maana ya jina lake jipya ilikuwa —

Je! unaweza kumwambia mwalimu wako kwamba Ahadi Kuu ya Mungu kwa Israeli ilikuwa nini?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi; na neema kuliko fedha na dhahabu.” Mithali 22:1

Wakati Yakobo alipopewa jina jipya, alifurahi sana. Aliona fahari juu ya jina hilo kwa sababu lilionyesha upendo wa Mungu kwake. Alitaka kumtii Mungu na kuliletea utukufu jina hilo jipya ambalo Mungu alimpa.

Sisi sote tuna majina yetu. Je! tukifanya mambo mabaya watu watafikiri nini juu ya majina yetu? Ni lazima tumtii Mungu ili majina yetu yasifiwe.

Je! tunapokea majina mapya? Wakati tunapookolewa, tunajulikana kwa jina la “Wakristo.” Tunaitwa kwa jina la Kristo. Je! Bwana wetu angekasirika kama tungefanya maovu na kuwafanya watu kufikiria jina lake mambo mabaya?



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Nne

YUSUFU ABADILI HISTORIA YA WAEBRANIA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 37:1-4; Mwanzo 41:46-57; Mwanzo 46:1-7, 28-34; Mwanzo 50:15-22

Yusufu alikuwa mmojawapo wa wana wa Yakobo. Alikuwa na ndugu zake wakubwa na ndugu mmoja mdogo wake aliyeitwa Benjamini. Yusufu na Benjamini walikuwa wana wa Raheli mke wa Yakobo ambaye Yakobo alimpenda sana. Yusufu na Benjamini pia walipendwa sana na baba yao.

Yakobo alimpenda Yusufu zaidi kuliko wanawe wote. Alimpa Yusufu vazi lililokuwa zuri zaidi kuliko mavazi yao ndugu zake. Yusufu alikuwa mtoto mpole na mtiifu. Wakati mwingine alisaidia kuchunga kondoo, lakini kwa kawaida alikaa nyumbani karibu na baba yake. Alimpendeza baba yake sana.

Wakati ndugu za Yusufu walipoona kwamba baba yao alimpenda sana, walimchukia. Hawakusema naye kwa upole. Siku moja Yusufu alimwambia baba yake matendo mabaya ambayo ndugu zake walifanya. Jambo hili

liliwafanya ndugu zake kumchukia zaidi. (Soma Mwanzo 37:5-11)



Baadaye kidogo nduguze Yusufu walimchukua, wakamwuuza kama mtumwa kwa wasafiri wengine. Wasafiri hawa, baadaye walimwuuza Yusufu Misri kwa mtu mmoja aliyeitwa Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari. Alipendezwa sana na kazi ya Yusufu. Lakini mke wake alikuwa mwovu na alimshuhudia Yusufu uwongo kwa mume wake. Potifa aliamini maneno ya mkewe kwa hivyo alimfunga Yusufu gerezeni.

Yusufu alikuwa bado kumsahau Mungu. Hakuwa na hatia yo yote. Alipokuwa gerezani, aliaminiwa sana. Bwana alikuwapo pamoja naye hata gerezani.



Baadaye kidogo, mtumishi (mnyweshaji) wa mfalme na mpishi wake (mwokaji) walifungwa gerezani kwa kumkosea mfalme. Wote wawili waliota ndoto juu ya mambo ambayo yangetokea. Mungu alimwambia Yusufu maana ya ndoto zile, kisha Yusufu aliwatafsiria. Mambo waliyoota yalifanyika hasa kama Yusufu alivyowatafsiria.

Siku moja, mfalme aliota ndoto. Ndoto hii ilimfanya mtumishi wa mfalme kumkumbuka Yusufu. Alimwambia mfalme jinsi Mungu alivyomwambia Yusufu maana ya ndoto. Farao alimwita Yusufu, kisha Yusufu alimtafsiria maana ya ndoto zake.

Ndoto za mfalme zilionya juu ya njaa ambayo ingetokea. Mungu ali-

mwambia Yusufu mambo ambayo watu wangepanya ili kujitayarisha kwa njaa hiyo. Farao aliona kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yusufu, kwa hivyo alimfanya Yusufu kuwa mtawala katika Misri.

Yusufu alitayarisha Misri kwa njaa, lakini katika nchi nyingine watu waliteseka sana. Nduguze Yusufu walisafiri kwenda Misri kujaribu künunua chakula (nafaka). Hata hawakumtambua Yusufu.

Yusufu alijifanya kuwa alikasirika na ndugu zake. Aliwaambia kwenda kumleta Benjamini ndugu yao mdogo kwanza ndipo angewauzia chakula. Kisha alijitambulisha kwao kwamba alikuwa ndugu yao, na kwamba hakukasirika. Aliwaambia kwamba Mungu alitumia uovu waliomtendea kuokoa jamaa ya Israeli katika mateso ya njaa.

Ndugu hawa waliojaa furaha walimleta Yakobo baba yao kukaa na Yusufu Misri. Mungu alionyesha kwa



mara nyingine tena kwamba alikumbuka ahadi yake kwa Yakobo ambaye sasa aliitwa Israeli.

KAZI YA KUFANYA:

Chora mstari kutoka kwa jina la Yusufu hadi kwa sababu zilizowafanya ndugu zake kumchukia.

Yusufu

alikuwa mkubwa na alikuwa na nguvu nyingi zaidi kuliko ndugu zake.

alipendwa zaidi na baba yake kuliko ndugu zake.

alipewa mavazi mema na baba yake.

mara kwa mara alichaguliwa kuchunga kondoo.

alimwambia baba yao wakati ndugu zake walipotenda kosa.



Kifungu cha _____.



Kifungu cha _____.



Kifungu cha _____.

Kamilisha hadithi ifuatayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa.

Mfalme wa Misri aliota ndoto iliyomwonya kwamba _____ ingetokea. Mfalme alimchagua _____ kuwa mtawala Misri kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye. Mungu alitaka Yusufu kuwa mtawala katika Misri ili angeokoa jamaa ya _____.

Soma Mwanzo 37:23-25. Chini ya kila picha andika namba ya kifungu cha Biblia kielezacho juu yake.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

**"Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheana kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi."
Waefeso 4:32**

Yusufu hakuogopa wakati ndugu zake walipomwuuza kama mtumwa. Alijua kwamba Mungu alikuwa pamoja naye. Hakuogopa wakati alipokuwa gerezani kwa sababu alijua kwamba Mungu angemtunza. Mungu alikuwa akiongoza maisha yake, na alimwamini. Hakufahamu mambo Mungu aliyokuwa akifanya, lakini alikuwa na imani.

Wakati mwingine tunaogopa. Hii inaonyesha kwamba hatumwamini Yesu kweli kututunza. Hata wakati tunapofikiri ya kwamba mambo mabaya yanatufanyikia, inatupasa kumwamini Yesu. Yesu anaweza kuongoza maisha yetu hata wakati ambapo hatufahamu mambo anayoyafanya. Anatumunza sikuzote.



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Tano

WAKATI WAEBRANIA WALIPOKUWA WATUMWA


MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 1:7-22; Kutoka 2:23-25; Kutoka 5:10-19

Wakati Yakobo babaye Yusufu pamoja na jamaa yake walipohamia Misri, waliruhusiwa kukaa mahali pazuri. Walipewa nchi ya Gosheni. Nchi hii walipewa na Farao kwa sababu Yusufu aliiokea Misri katika mateso ya njaa. Yakobo alikaa kwa furaha Misri kwa miaka kumi na saba, kisha alikufa.

Hata baada ya Yakobo kufa jamaa yake waliendelea kukaa Misri. Mungu alikwisha kuahidi kufanya jamaa ya Yakobo kuwa taifa kubwa, na hakika walianza kuongezaka kuwa taifa kubwa Misri. Yusufu na nduguze walikufa baada ya miaka mingi. Watoto wao walikaa Misri kwa amani kwa miaka mingi sana mpaka wakati Farao mpya alipoanza kutawala.

Farao huyu hakujali Waebrania. Aliona tu kwamba walikuwa taifa lenye nguvu, na kwamba walikaa katika nchi nzuri sana nchini Misri. Aliwaogopa.

Kisha Farao huyu aliwafanya Waebrania kuwa watumwa. Aliwaweka wengine katika kazi ngumu kumjengea miji ya kuwekea hazina yake. Walifanya matofali, wakayatumia kujengea ghala za nafaka na ngome. Waebrania wengi walifanya kazi mashambani. Farao aliwaweka kuwalazimisha kufanya kazi kwa nguvu



zaidi kupita kiasi. Waebrania hao waliadhibiwa wakati walipofanya kazi polepole au walipokosa kuitenda vyema.

Waebrania walianza kuwachukia Wamisri wenyeji wao. Walianza pia kusimulia hadithi nyingi juu ya nchi ambayo Mungu aliahidi taifa lao. Wazee walisimulia juu ya nchi ya Kanaani ambayo Waebrania walikaa zamani. Maisha yao yalikuwa ya uchungu sana wakati walipoteswa na Wamisri. Hakika, walifikiria kwamba siku moja Mungu angewatoa katika utumwa wao na kuwarudisha Kanaani. Walitumaini kwamba siku moja wangekuwa na mizabibu yao, miti yao, kondoo zao, mbuzi zao, na ng'ombe zao.

Waebrania walikuwa na huzuni sana. Walianza kumwomba Mungu. Walimwuliza kuwaokoa utumwani ili wangepewe kurudi katika nchi ya Kanaani. Hata kabla wao kuanza kuomba, Mungu alikuwa akifanya mpango kuwaokoa. Alisikia maombi yao. Alikuwa akifanya mpango ule alioanza kufanya zamani sana kwa Ibrahimu.

Farao alikuwa akifanya maisha kuwa magumu sana kwa Waebrania. Wana wa Israeli walikuwa wakiongezeka kuwa wengi. Wamisri waliogopa kwamba taifa la Waebrania lingekuwa na nguvu zaidi kuliko wao.

Farao alikata shauri kuwaua watoto wote wanaume wa Waebrania. Aliwaamuru wazalisha kufanya hivyo. Amri hiyo yake haikutimizwa kwa sababu wazalisha wengi walikuwa Waebrania na walimcha Mungu. Kisha Farao aliwaambia askari wake kuwatupa katika Mto wa Nile watoto

wote wanaume wa Kiebrania. Watoto wengi waliuawa na wengi waliishi.

Mtoto mmoja aliyeokolewa na Mungu katika mauti hayo alikuwa wa maana sana. Yeye ndiye Mungu alipanga kutumia kuwasaidia watu wake kukimbia kutoka Misri. Kwa kweli, Mungu hakupanga kuokoa Israeli kwa mtoto huyo, lakini angekua na kuwa mtu wa Mungu.



KAZI YA KUFANYA:

Waebrania waliruhusiwa kukaa katika nchi nzuri ya Gosheni kwa sababu _____ aliokoa nchi ya _____ katika njaa.

Wakati Waebrania walipoongezeka kuwa taifa lenye nguvu, na kukaa katika nchi nzuri, Wamisri waliwafanya kuwa _____.

Farao yule mwovu aliyewaogopa Waebrania aliamuru kwamba watoto wanaume wa Waebrania waliozaliwa watupwe _____. Lakini Mungu aliwaokoa wengi. Mtoto mmoja kati ya wale waliookolewa baadaye angekuwa kiongozi wa Waebrania. Aliitwa _____. Mungu alipanga kumtumia kuwasaidia _____ kutoka katika nchi ya Misri.


Andika majibu katika nafasi zilizoachwa katika mchezo huu wa fumbo. Andika herufi moja tu katika kila chumba.

Andika kutoka juu mpaka chini.

1. Ni watu gani waliokuwa watumwa katika somo hili?
3. Ni mtoto gani ambaye Mungu alipanga kuwaongoza watu wake kutoka katika utumwa?

Kujaza kuanzia kushoto hadi kulia.

2. Baba ya Yusufu alikuwa nani?
3. Watu wa Mungu walikuwa watumwa katika nchi gani?



Waebrania hawakukaa kwa furaha nchini Misri. Waliteswa sana kama watumwa. Walimwomba Mungu kuwaokoa. Wengi walifikiri ya kwamba Mungu aliwasahau au aliwaacha. Lakini Mungu hakusahau ahadi yake. Alikuwa akipanga kuwaokoa baada ya wao kuwa taifa lenye nguvu. Aliwapa Musa kama kiongozi kuwaokoa.

Mungu hatusahau wakati ambapo tuko katika taabu. Anatupenda na anatutunza. Alimtuma Yesu Kristo kutuokoa katika dhambi na kuwa Mwokozi wetu. Tunaweza kumwamini Mungu na kujua kwamba anaongoza maisha yetu. Kwa hakika, Yesu anatutunza.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mliyoyavyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, 'Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa'." Waebrania 13:5



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Sita

MUSA ASIKIA MWITO WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 2:11-25; 3:1-20 Kutoka 4:1-5:1

Hadithi juu ya mtoto Musa imekwisha kusimuliwa mara nyingi sana. Labda umekwisha kusikia jinsi dada ya Musa alivyomtia ndani ya kisafina cha manyasi, akamficha katika maji kando ya mto ili kuokoa maisha yake. Alikotwa na binti Farao. Binti huyo alimchukua, akataka kumfanya kuwa mtoto wake, kwa hivyo Musa alilelewa katika makao ya mfalme Farao.

Mamaye Musa ndiye aliyekuwa mlezi wake katika makao ya mfalme wakati alipokuwa mtoto. Alifundisha habari za Waebrania na za nchi ya Kanaani. Bila shaka mamaye Musa alimfundisha habari za Mungu na Ahadi yake kwa Ibrahimu na kwa Yakobo. Labda Musa alijiona moyoni mwake kwamba Mungu alimtaka kuwasaidia Waisraeli. Lakini wakati ule hangaliweza kujua jinsi Mungu angemtumia katika kusudi lake.



Musa alikaa kama mtoto wa binti Farao. Alikuwa na nafasi nyingi. Alisoma katika shule nzuri sana na vyyo vikuu katika Misri. Angepokea urithi wake katika jamii ya kifalme wakati ambapo angekuwa mkubwa.

Lakini mambo haya yote hayakumridhisha Musa. Aliwaona Waisraeli (Waebrania) watu wake,

wakiteswa, na aliwaza moyoni mwake kwamba ilimpasa kuwasaidia katika njia fulani. Hangeweza kuwa Mmisri. Alijua kwamba alikuwa Mwebrania.

Siku moja, Musa alimwona Mmisri akimpiga Mwebrania mmoja mtumwa. Alikasirika sana. Alimwua Mmisri yule mkatili akifikiri kwamba Waebrania wangepahamu kwamba alikuwa akiwasaidia. Lakini hawakufahamu.



Siku ya pili, Musa aliwaona Waebrania wawili wakipigana. Aliwaambia kuacha kupigana. Mmoja wa Waebrania wale waliokuwa wakipigana alimwuliza kama alitaka kumwua kama alivyomwua Mmisri yule. Musa alitambua kwamba jambo lile alilofanya lilijulikana. Baada ya muda mfupi Farao angejua jambo lile.

Alikimbia kabla ya Farao kujua akaenda katika nchi ya Midiani iliyokuwa upande mwingine wa jangwa.

Musa alitumikia kama mchungaji kwa muda wa miaka arobaini. Aliwachunga kondoo katika jangwa lililokuwa karibu na Midiani. Alioa binti ya Yethro aliyemtumikia.

Wakati Musa alipokuwa mchungaji alikuwa na wakati kufikiria mambo mengi. Alikumbuka mambo yote ambayo mama yake alimfundisha juu ya Waebrania. Alifikiria mambo yote aliyojifunza katika shule za Wamisri. Pia, alifikiria imani yake kuu kwa Mungu.

Musa alijifunza kukaa jangwani. Alijifunza pia jinsi ya kupata njia yake bila kupotea jangwani. Alijifunza jinsi ya kupata maji na jinsi ya kujikinga na wanyama wa mwitu.

Musa hakujua kwamba Mungu alikuwa akimtayarisha kuwaongoza Waisraeli. Lakini Mungu alijua, na alikuwa akifanya mpango.

Katika wakati huu wote, Waisraeli walikuwa utumwani. Walikuwa wakiteswa. Kila siku walimlilia Mungu kuwasaidia. Hakika, Mungu aliwasikia. Mungu alikumbuka ahadi yake kwa Ibrahimu, kwa Isaka, na kwa Yakobo. Hangewaacha watu wake. Alikuwa akiwatayarishia kiongozi ili mpango wake ungeweza kutimizwa.

Musa alishangaa sana siku moja. Aliona kijiti jangwani kikiwaka moto. Alipokitazama, aliona kwamba hakikuteketea. Aliposongea karibu, Mungu alisema naye kutoka katikati ya kijiti kile.



Mtoto Musa aliokotwa na _____ . (Mamaye, binti Farao, jeshi la mfalme, malaika)

Musa alikimbia kutoka Misri kwa sababu _____. (alimwua mtu, hakuwa Mmisri, mama yake alimfukuza)

Wakati Mungu alipomtuma Musa kurudi Misri, alimtokea katika _____. (Mawingu meupe, moshi, mwali wa moto mbinguni, kijiti kiwakacho moto)

Chora mstari kutoka kwa kila jina hadi kwa maneno yanayozungumzia habari zake.

- | | |
|----------------|--|
| 1. Musa | A. Alimchukua mtoto kukaa naye katika makao ya mfalme. |
| 2. Binti Farao | |
| 3. Mungu | B. Alitaka kuwasaidia watu wake. |
| 4. Yethro | C. Musa alioa binti yake. |
| 5. Mmisri | |
| 6. Farao | D. Alisema na Musa kutoka katikati ya kijiti kilichowaka moto. |
| | E. Alikuwa mkali sana. |
| | F. Alimpiga Mwebrania. |

Mungu alisema ya kwamba alikwisha kusikia maombi ya wana wa Israeli. Alimwambia Musa kwenda kwa Farao kumwambia kuwaruhusu Waebrania kurudi Kanaani. Musa aliogopa, na hakujiona kuwa na nguvu za kutosha kufanya mambo ambayo Mungu alimwambia.

Mungu alimkumbusha Musa kwamba angekuwa pamoja naye wakati wote kumtia nguvu. Pia, alimwambia Musa ya kwamba Farao hangewaruhusu Waebrania kuondoka mpaka nguvu zake zingemlazimisha kufanya hivyo.

Musa alikwenda kwa Yethro mkwewe, akamwambia mambo yote ambayo Mungu alimwambia kufanya. Aliondoka Midiani, akasafiri kurejea Misri kupitia jangwani.

KAZI YA KUFANYA:

Chagua jibu lililo kweli katika majibu yafuatayo na kuliandika katika mstari ulioachwa.

Ili kuokoa maisha ya Musa, mama yake alimtia katika _____ (pango, nyumba yake, kisafina cha manyasi, makao ya mfalme)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

**“Bwana yu karibu na wote
wamwitao, wote wamwitao kwa
uaminifu.” Zaburi 145:18**

Mungu alimchagua Musa kuwaokoa Waebrania katika Misri. Kwanza, Musa hakuelewa uongozi wa Mungu. Hata alimwua Mmisri ili kuwasaidia watu wake. Lakini tendo hilo halikuwa la Mungu. Wakati Musa alipokimbia kutoka Misri, labda alifikiri kwamba aliwaacha watu wake. Lakini Mungu alikuwa akifanya mpango wake.

Mungu ana mpango wa ajabu kwa kila mmoja wetu. Wakati mwingine hatufahamu mpango huo. Tunaweza kufikiri kwamba tumeshindwa. Lakini Mungu atafanya kazi katika maisha yetu kama tutamwomba kufanya hivyo.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Saba

WAEBRANIA WASAFIRI KUELEKEA KANAANI

MASOMO YA BIBLIA: Kutoka 13:17-22; Kutoka 14:1-17:6

Musa alichukua jamaa yake, wakarejea Misri. Alibeba fimbo aliyopewa na Mungu mkononi mwake. Mungu aliahidi kwamba angemsaidia Musa kuwatoa wana wa Israeli katika nchi ya Misri. Musa alimwamini Mungu.

Musa alijua kwamba Farao hangewaruhusu Waisraeli (Waebrania) watumwa kuondoka Misri kwa urahisi. Alijua kwamba Mungu ndiye angemlazimisha Farao kuwaruhusu wana wa Israeli kuondoka. Mungu alimwahidi Musa ya kwamba kwa fimbo ile aliyokuwa nayo, angefanya mambo mengi ya ajabu. Musa alijua hakika ya kwamba Mungu hangeacha kutimiza kusudi lake kwake.

Musa alipokuwa akisafiri, alikutana na Haruni ndugu yake. Mungu alikwisha kumwambia Haruni kwenda pamoja na Musa. Musa alijua kwamba Haruni angemsaidia kuwatoa wana wa Israeli katika nchi ya Misri.

Wakati Musa na Haruni walipofika Misri, waliwakusanya wazee wote wa wana wa Israeli. Waliwaambia jinsi Mungu alivyosema, na kwamba wana wa Israeli wangukuwa huru. Watu waliamini wakati walipoona uwezo wa Mungu katika Musa na Haruni.


Waebrania walimsifu Mungu kwa sababu alisikia maombi yao. Walijua kwamba Mungu angewaokoa katika utumwa.

Habari hii ilikuwa njema, lakini hatimaye angemshurutisha Farao kuwaruhusu wana wa Israeli kuondoka. Musa na Haruni walianza mara moja kumjulisha Farao habari hii.

Walimwendea Farao, waka-mwambia kwamba Mungu aliwataka wana wa Israeli kwenda kumwabudu jangwani. Lakini Farao hakumjua Mungu, kwa hivyo hakuwaruhusu wana wa Israeli kuondoka.


Wakati Musa na Haruni waliposisitiza kwamba wana wa Israeli waondoke, Farao alikasirika.

Aliwaamuru Musa na Haruni kufanya kazi, kisha aliifanya kazi ya Waebrania kuwa ngumu zaidi kuliko vile ilivyokuwa.



Wana wa Israeli walilia sana juu ya mateso yao. Musa alisema na Bwana juu ya mateso hayo. Mungu akawakumbusha juu ya Ahadi yake kwa Ibrahimu, kwa Isaka na kwa Yakobo. Alimwambia Musa kuwa na imani. Farao hangeweza kuwaruhusu wana wa Israeli kuondoka mpaka wakati ambapo angeona mambo ya ajabu na nguvu za Bwana.

Basi, Bwana alituma misiba (au mateso) kumi katika nchi ya Misri.



Wakati huu ulikuwa wa taabu. Msiba wa kwanza ulikuwa wa vyura waliokuwa juu ya nchi yote ya Misri. Wakati wa kila msiba, Farao aliahidi kuwaruhusu wana wa Israeli kuondoka kama Mungu angeondoa msiba huo. Lakini Mungu alipoondoa msiba, Farao alikataa kuwaruhusu wana wa Israeli kuondoka.

Hatimaye Mungu aliwaonya watu kwamba angetuma msiba mbaya zaidi kuliko misiba yote. Musa na Haruni waliwaambia wana wa Israeli mambo waliyopaswa kufanya wasipatwe na madhara yo yote wakati msiba ule ungekuwa juu ya nchi yote ya Misri.

Ulipokuwa usiku wa manane, Mungu alituma msiba huo. Kulikuwa na mauti katika kila nyumba ya Mmisri. Mzaliwa wa kwanza wa kila jamaa ya Wamisri alikufa, hata nyumbani mwa Farao mwenyewe. Lakini Waebrania walikuwa salama kwa sababu walimtii Mungu.

Wakati Farao alipoona uwezo huu wa Mungu, aliwaita Musa na Haruni kwake. Aliwaambia kuwachukua watu wao na kuondoka. Hakungojea mpaka ilipokuwa asubuhi. Aliwaambia kuchukua ng'ombe, kondoo, na mbuzi zao.

Waebrania walikuwa tayari kuondoka. Mungu aliwaambia kujitayarisha ili wangeondoka upesi. Walitembea kutoka Misri, wakaingia jangwani. Walikuwa na furaha nyingi wakiimba nyimbo za kumsifu Mungu. Walikuwa wakienda Kanaani, Nchi ya Ahadi.



Askari wa Farao waliwafuata wana wa Israeli, lakini Mungu aliwalinda. Mungu aliwafanyia wana wa Israeli nchi kavu katika Bahari ya Shamu, wakapita, lakini Mungu aliyarudisha maji, yakafunikiza Wamisri wote, wakafa.

Baadaye kidogo jangwa likawa na njoto jingi, ikawa vigumu kupata maji. Watu walianza kutamani kuona mashamba mema ya Misri. Walinung'unika. Lakini Mungu aliwalinda watu wake. Aliwapa maji. Aliwaonyesha upande uliowapasa kwenda. Mungu alikuwa akifanya mpango wake kwa watu wa Israeli. Alikuwa akitimiza ahadi yake alioahidi zamani sana.

KAZI YA KUFANYA:

Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika majibu yako katika mistari.

Je! Mungu alimpa Musa kitu gani cha kufanyia mambo ya ajabu?

Je! Mungu alimtuma nani pamoja na Musa kumsaidia? _____

Waebrania hawakupatwa na dhara lote la misiba kwa sababu _____

Chora mstari hadi kwa majibu ya kweli:

kufanya njia katika bahari.

Mungu aliwa- kuwaonyesha upande
tunza watu wa kwenda.
wake kwa kuwapa maji.

walimwamini kila siku.

Watu wa walinung'unika
Mungu wakati wa taabu.

waliimba nyimbo za kumsifu hata wakati wa huzuni.

walirudi Misri.

VIFUNGU VYA KUKUMBUKA:

"Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huni-ongoza. Hunihuisha nafsi yangu; na kunilongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji." Zaburi 23:1-4

Wakati mwingine Waebrania walinung'unika. Walifikiri kwamba wakati mwingine Mungu hakuwalinda vyema. Lakini Mungu aliendelea kuwapenda na kuwalinda. Wakati walipokuwa na njaa, Mungu aliwalisha. Wakati walipokuwa na kiu, Mungu aliwapa maji ya kunywa. Mungu aliwaongoza njiani mpaka wakafika katika Nchi ya Ahadi.

Kila siku Mungu anatusaidia. Chakula chetu na maji tunayokunywa yanatoka kwa Mungu. Wakati mwingine tunakuwa na huzuni. Tunaweza kulalamika. Labda tunaweza kufikiri ya kwamba Mungu hatupendi. Hii si kweli. Inatupasa kukumbuka kumshukuru Mungu kila siku kwa mambo yote anayotupa. Kisha tutaona kuwa anatupenda kiasi gani.



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Nane

KATIKA MLANGO WA NCHI YA AHADI

MASOMO YA BIBLIA: Hesabu 13 na 14

Labda inaweza kuonekana kwamba njia iliyokuwa nzuri kuingia katika Nchi ya Ahadi ilikuwa ya kuvuka jangwa. Waebrania hawakufuata njia hii. Kulikuwa na makabila yenye nguvu ambayo pengine wangewapiga Waisraeli na kuwateka. Mungu alijua kwamba watu wake walihitaji wakati kuwa wenye nguvu na kujifunza kumwamini. Kwa hivyo walifuata njia nyingine.



Walisafiri kuelekea kusini karibu na Bahari ya Shamu. Huko kusini walipata Mlima wa Sinai. Katika Mlima huo wa Sinai ndipo Waisraeli walipokea Amri Kumi za Mungu. Kisha waliendelea na safari kuelekea Nchi ya Ahadi. Walisafiri upande wa mashariki ya kaskazini, wakatembea maili nyingi mpaka wakafika Kadeshi.

Kadeshi ilikuwa karibu sana na Nchi ya Ahadi. Bila shaka Waisraeli walikuwa na furaha ya kwamba walikuwa karibu kumaliza safari yao. Musa aliwatuma wapelelezi kama Mungu alivyomwamuru. Wapelelezi hao walikwenda kuichunguza Nchi ya Ahadi, wakarejea, wakawaambia watu pamoja na Musa mambo waliyoyaona.

Waisraeli walitaka kujua kama kulikuwa na habari njema kutoka huko. Walitaka kujua kama kulikuwa na maji mengi huko. Je! wenyeji wa Nchi hiyo ya Ahadi walikuwa wengi na wenye nguvu? Je! miji yao ilikuwa na kuta zenye nguvu? Waisraeli bado walikuwa na shaka kama kweli Mungu alijua mambo yaliyokuwa mema kwao.

Mtu mmoja mkuu kutoka kila kabila alitumwa kwenda kupeleleza. Waliipeleleza Nchi ile ya Ahadi wakaiona kuwa nzuri. Kulikuwa na mazao mengi, mito, watu wenye nguvu, na miji iliyozungukwa na ukuta.



Walakini, wapelelezi walirejea na maelezo mawili tofauti ya mambo waliyoyaona.

Wapelelezi hao walikaa katika Nchi ya Ahadi kwa muda wa siku arobaini. Wote walisema kwamba Nchi ile ilijaa matunda. Lakiŋi wengi wao walisema kwamba Waisraeli hawangeweza kuwapiga wenyeji wa Nchi ile. Hawakumwamini Mungu kuwapigania vita. Walikuwa waoga.

Wapelelezi wawili tu ndio waliokataa kukubali maneno hayo, nao walikuwa Yoshua na Kalebu. Waliona Nchi ile nzuri ambayo Mungu aliahidi. Waliamini kwamba Mungu angewapa.

Walisema, “Na tupande mara, tukaitamalaki.” (Hesabu 13:30)

Waisraeli waliamini habari ile mbaya iliyoletwa na wapelelezi waoga. Walimnung'unikia Mungu na walikataa kumtii.

Hakika, Mungu alisikia mambo haya yote na yalimkasirisha sana. Alisema na Musa, akamwambia ya kwamba angechagua kundi lingine la watu badala ya hawa kuingia katika Nchi ya Ahadi. Lakini Musa aliwapenda Waisraeli sana na alimwomba Mungu kuwasamehe.

Mungu hakuwaruhusu wenye dhambi kuingia katika nchi ile mpya. Alisema kwamba Waisraeli wangezunguka jangwani kwa muda wa miaka arobaini mpaka wazee wote walionung'unika wangekufa ndipo wangeingia katika Nchi ya Ahadi. Wapelelezi waliokuwa wema, yaani, Yoshua na Kalebu, pia walizunguka jangwani lakini Mungu aliahidi kwamba wao wangeingia katika Nchi ya Ahadi.

KAZI YA KUFANYA:

Jaza nafasi zilizoachwa:

Mungu aliwapa Waebrania _____ katika Mlima wa Sinai.

Waebrania waliwatuma _____ katika Nchi ya Ahadi kuiona kama ilikuwa nzuri.

Yoshua na Kalebu walikuwa wapelelezi wema, na wangezuka kuitwaa Nchi ya Ahadi kwa sababu waliamini kwamba _____ ange-wasaidia.

Wapelelezi wengine walisema kwamba Nchi ya Ahadi ilikuwa nzuri, lakini _____ kuingia humo.

Je! unaweza kumwambia mwalimu wako mambo Mungu aliyowaambia Waebrania kuwa yaliwapasa kufanya kwa sababu hawakumwamini? _____

Andika herufi "K" kando ya sentensi ambayo ni kweli na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

Tusisahau kujua kwamba Mungu anatupenda. Haitupasi kuogopa. Mungu anataka kutulinda na atatupigania vita vyetu kama tutamwomba.

Je! vita vyetu ni nini? Ni shida zote tulizo nazo na vitu vinavyotutisha. Ni majaribu yanayotujia.

- _____ 1. Wapelelezi wote walisema kwamba wangepiga vita Nchi ya Ahadi.
- _____ 2. Wapelelezi walisema kwamba ilikuwa nchi, nzuri.
- _____ 3. Wapelelezi wawili waliamini kwamba Mungu angewasaidia watu wake.
- _____ 4. Watu walikuwa na imani katika Mungu.
- _____ 5. Waisraeli walizunguka jangwani kwa sababu wali-kuwa na shaka na Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msilogope wala msiwahofu; kwa maana Bwana, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe; hatakupungukia wala kukuacha."
Kumbukumbu la Torati 31:6

Wakati Waebrania walipofika katika Nchi ya Ahadi, waliogopa. Waliogopa kwa sababu hawakumwamini Mungu. Walifikiri kwamba wangepigana vita wao wenyewe. Walisahau kujua kwamba Mungu alikuwa pamoja nao, na kwamba angewapigania vita.



VIJANA TUIJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Tisa

WAEBRANIA WAINGIA KWAO KANAANI

MASOMO YA BIBLIA: Kumbu-kumbu la Torati 5:1-33; 6:4,5; 31:1-13; 34:1-12; Yoshua 1:1-3:17; 4:13-24; 6:1-16,20

Wana wa Israeli walikwisha kuzunguka jangwani kwa miaka mingi. Sasa walipiga kambi yao karibu na Mto wa Yordani. Baada ya muda mfupi wangevuka Mto huo kuingia katika Nchi ya Ahadi. Siye Musa aliyekuwa akiwaongoza wana wa Israeli sasa. Alikwisha kufa miaka mingi iliyopita. Wana wa Israeli walikuwa na kiongozi mpya sasa aliyeitwa Yoshua.

Walikumbuka jinsi walivyongojea zamani kwa hamu kubwa kuingia katika Nchi ya Ahadi. Walikumbuka jinsi baba zao walikuwa na imani haba kwa Mungu. Walikumbuka jinsi Mungu alivyowarudisha jangwani.

Mungu aliwaongoza wana wa Israeli jangwani kwa muda wa miaka arobaini. Walifuata wingu lake mfano wa nguzo mchana, na moto mfano wa nguzo usiku. Walikuwa katika imani yao wakati waliposafiri. Waliwafundisha

watoto wao kumheshimu Mungu. Lakini bado walinung'unika wakati mambo hayakuwaendelea vyema. Waliona shaka mara moja juu ya Mungu wakati walipokuwa na shida.

Zamani, wakati wana wa Israeli waliponung'unika, Musa alikasirika sana. Wakati Mungu alipowapa wana wa Israeli maji, Musa aliwaruhusu kumsifu yeye badala ya kumsifu Mungu. Mungu alimwadhibu Musa kwa dhambi hii. Alimwambia kwamba hangeingia katika Nchi ya Ahadi.


Bila shaka Musa alikuwa na huzuni lakini hakunung'unika. Aliwaongoza wana wa Israeli jangwani na aliwafundisha. Wakati alipokuwa jangwani aliandika Kitabu cha Torati.

Musa aliiona Nchi ya Ahadi. Mungu alimwonyesha nchi ile nzuri ya Waisraeli kutoka juu ya mlima mrefu. Kisha alikufa. Yoshua alichaguliwa kuwa kiongozi wa wana wa Israeli. Yoshua alikuwa mmoja wa wapelelezi waliotumwa kuipeleleza Nchi ya Ahadi

miaka mingi iliyopita. Alionyesha imani yake kwa Mungu na watu walimheshimu sana.

Sasa, wana wa Israeli walikuwa wakingojea amri ya Bwana kuvuka Mto wa Yordani. Yoshua aliwatuma wapelelezi wawili katika nchi ile, na waliporejea, walimpasha habari njema. Walijua ya kwamba Mungu angewapa ushindi. Yoshua aliwaambia watu kuwa tayari kuvuka Mto wa Yordani siku ya pili yake. Mto huo ulikuwa umejaa maji mengi lakini watu hawakuuliza jinsi wangevuka ng'ambo ya pili.

Ilipopambazuka, Mto wa Yordani bado umejaa maji. Makuhani walibeba sanduku la agano la Mungu mpaka ukingoni mwa mto, kisha walitia nyayo



zao katika maji ya Yordani. Mungu alisimamisha maji, watu wakapita katika nchi kavu kama baba zao walivyovuka Bahari ya Shamu. Walifanya madhabahu (yaani,

walikusanya mawe mengi0 ya kuwakumbusha mwujiza huu wa Mungu aliowafanyia.

Waebrania hawakuweza kukaa kwa amani katika Nchi ya Ahadi mpaka wanguwashinda maadui zao kabisa. Karibu nao palikuwa na mji wa Yeriko. Mji huo ulikuwa salama maana ulizungukwa na kuta na milango yenye nguvu.

Lakini kuta na milango hazingeweza kuzuia mpango wa Mungu kufanya kazi. Mungu alimpa Yoshua mpango wake na Yoshua alijua kwamba Mungu angejipatia ushindi tena. Watu hawakuogopa wala hawakuwa na shaka juu ya Mungu. Walitembea kuzunguka mji huo wa Yeriko na Mungu aliutia mikononi mwao. (Soma Yoshua 6.)

Baada ya muda mchache, Nchi ya Ahadi ilikuwa mikononi mwa wana wa Israeli. Iligawanywa kati ya makabila kumi na mawili. Baada ya muda sio mrefu, wana wa Israeli walikaa katika nchi ya o mpya.

Yoshua alijua kwamba wakati wake wa uongozi ulikwisha. Aliwaita Waebrania wote pamoja, akawaaga. Walimwahidi kuendelea kuwa waaminifu kwa Mungu. Baada ya hayo, Yoshua alikufa. Waebrania walitumikia Mungu kwa uaminifu kwa miaka mingi sana.

KAZI YA KUFANYA:

Kiongozi mpya wa Waebrania alikuwa_____.

Musa _____ Nchi ya Ahadi lakini hakuweza _____ katika nchi hiyo.

Wakati Musa alipokuwa jangwani,
aliandika Vitabu vya _____ .

Waisraeli walipomwamini Mungu,
Mungu aliwafanyia nchi kavu katika
_____ .

Wakati Waisraeli walipomwamini
Mungu, aliwashindia mji wa_____ .

Chora mstari hadi kwa jibu la kweli.

Mungu aliwaongoza watu wake mchana kwa	moto mfano wa nguzo.
--	-------------------------

Mungu aliwaongoza watu wake usiku kwa	makabila kumi na mawili.
--	--------------------------------

Musa aliona lakini hakuweza kuingia katika	wingu mfano wa nguzo.
--	--------------------------

Wana wa Israeli wali- gawanyika katika	Mto wa Yordani.
---	--------------------

Walivuka katika nchi kavu katika	Nchi ya Ahadi.
-------------------------------------	-------------------

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

**“Bwana ndiye aliyewafukuza watu
wa mataifa yote watoke mbele yetu,
naam, Waamori waliokaa katika
nchi hii; basi, kwa sababu hiyo sisi
nasi tutamtumikia Bwana; maana
yeye ndiye Mungu wetu.” Yoshua
24:18**

Mungu aliwachagua watu wema
kuwaongoza watu wake. Aliwachagua
watu waliomheshimu. Waisraeli mara
kwa mara walilalamika juu ya viongozi
wao na juu ya Mungu. Lakini Mungu
aliwasamehe na aliwaongoza kuingia
katika Nchi ya Ahadi.

Tuna viongozi katika serikali yetu **na**
katika makanisa yetu. Inatupasa
kuwaheshimu viongozi hawa **na**
kuwaombea. Tukiwa na viongozi
wanaomheshimu Mungu, maisha yetu
yanakuwa ya furaha na nchi yetu
itakuwa na amani. Tukitaka nchi yetu
kuwa halisi kwa Mungu, ni lazima
tufanye mambo mawili. Ni lazima
tuombe ili viongozi wetu wamheshimu
Mungu, na ni lazima tumheshimu
Mungu sisi wenyewe.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Kumi

BAADHI YA WAEBRANIA WAAMUZI

MASOMO YA BIBLIA: Waamuzi 4:4-24; 5:1; 7:1-23; 16:23-31

Mungu aliwaamuru Waisraeli kuwafukuza mataifa yote ya wapagani waliowazunguka. Hata baada ya Yoshua kufa, vita viliendelea na Mungu aliwasaidia. Walakini, hawakuwafukuza watu wote kama walivyoamriwa na Mungu. Waliacha kupigana vita na maadui zao baada ya muda mfupi.

Waebrania waliruhusu watu wasio na dini kukaa nao katika Nchi ya Ahadi. Mungu aliwaonya kwamba wangekuwa na taabu kama wangeendelea kukaa na watu hao kwa sababu wangeabudu sanamu zilizotengenezwa kwa miti, mawe, dhahabu, na fedha.

Waebrania walitubu, lakini baada ya muda mfupi walisahau ahadi zao kwa Mungu. Hawakuwaruhusu watu hao wasio na dini kukaa nao tu, bali pia walifanya urafiki nao. Waebrania wengine walioa wanawake wa watu hao, kadhalika watu hao pia walioa wanawake wa Kiebrania. Baada ya muda usio mrefu, Waebrania walikuwa

wakiabudu sanamu pamoja na jamaa na marafiki zao wasio na dini.

Wana wa Israeli walikwisha kusikia mara nyingi ya kwamba palikuwa na Mungu mmoja tu wa kweli. Walijua kwamba haikuwapasa kumwabudu mtu ye yote. Wengi wao walijua Amri Kumi za Mungu kwa moyo. Lakini walipoanza kuabudu sanamu, walivunja sheria nyingi za Mungu.

Sanamu hizo za watu wasio na dini zilikuwa rahisi kuabudu. Hazikuwa na sheria zilizokuwa ngumu kuzifuata. Waisraeli walikata shauri kufanya kama majirani zao walivyofanya. Walikata shauri kujipendeza wao wenyewe badala ya kumpendeza Mungu. Walisahau sheria za Mungu na maonyo ya Musa.

Bwana aliwakasirikia sana watu wake. Aliwaruhusu maadui zao kuwashinda vitani. Waebrania walifanywa kuwa watumwa wa watu wale wasio na dini. Kisha walisikitika sana, wakamlilia Mungu. Mungu alisikia kilio chao na aliwapa waamuzi

kuwaongoza kupigana na maadui zao na kupata uhuru wao tena.

Waebrania walifanya hivyo mara kwa mara. Kwa muda wa miaka mia tatu Waebrania hawakujifunza mambo ambayo Mungu alikuwa akiwafundisha.

Kwanza, walitenda dhambi na kufuata miungu wa uwongo. Kisha maadui zao waliwashinda. Walimlilia Mungu, Mungu akawaokoa. Kisha tena walifuata miungu wa uwongo. Waliendelea kufanya hivyo tena na tena.

Mungu aliwatuma waamuzi au viongozi wa vita kumi na watano wa miaka mia tatu. Kila wakati Waebrania walipopata ushindi, walimsahau Mungu. Leo tutajifunza juu ya waamuzi watatu kati ya waamuzi wale kumi na watano.

DEBORA:



Wakati Waisraeli walipotenda dhambi, Mungu alimruhusu Yabini mfalme wa Kanaani kuwashinda. Waisraeli walimtumikia Yabini kama watumwa kwa muda wa miaka ishirini kabla Mungu kuwapa mwamuzi.

Mungu alimchagua Debora, nabii mke, aliyekaa chini ya mtende karibu na Betheli kuwa mwamuzi wao.

Debora alimwita Baraka aliyekuwa kiongozi shujaa wa Israeli, akamwambia kushambulia jeshi la Yabini. Baraka aliogopa. Alimtaka Debora kwenda pamoja naye vitani. Debora alimwambia Baraka ya kwamba amiri wa jeshi la Kanaani angeuawa na mwanamke.

Mungu aliwapa Waisraeli ushindi. Sisera aliyekuwa amiri wa jeshi la Kanaani, alikimbia kuokoa maisha yake. Baraka alimfuata akitaka kumwua. Sisera aliifikia hema ya mwanamke mmoja aliyeitwa Yaeli. Mwanamke huyu alimpa Sisera chakula na maji ya kunywa. Sisera alifikiri ya kwamba alipata kimbilio salama katika nyumba ya mwanamke huyu, kwa hivyo alilala usingizi. Wakati alipokuwa akilala, Yaeli alimwua kama Debora alivyotabiri. Wakati Baraka alipofika, alimkuta Sisera kama amekwisha kufa wala yeye hakumwua.

GIDEONI:

Baada ya miaka arobaini ya amani, Waisraeli walitenda dhambi tena. Wakati huu Mungu aliwaruhusu Wamidiani kuwashinda Waisraeli. Wamidiani hao walitwaa mazao ya shamba, ng'ombe, na kondoo za wana wa Israeli. Wana wa Israeli walijificha katika mapango yaliyokuwa milimani. Walimlilia Bwana tena, lakini kwanza Bwana alimtuma nabii kuwaambia dhambi yao na jinsi walivyoadhibiwa kwa ajili ya dhambi hiyo.

Baadaye Mungu alimchagua Gideoni kuwa mwamuzi. Alikuwa akipepetana ngano wakati alipojificha kutoka

machoni pa Wamidiani. Bwana alimwambia kuwaongoza wana wa Israeli kupigana na Wamidiani, kisha wangekuwa huru. Gideoni alimwamini Mungu, akamtolea sadaka ya kuteketezwa kama shukrani kwake. Kisha Gideoni alipiga tarumbeta kuwakusanya Waebrania wote pamoja. Alikusanya jeshi la askari elfu thelathini na mbili.

Mungu alimwambia Gideoni ya kwamba alikuwa na watu wengi mno. Alimwonyesha jinsi ya kuwachagua watu waliofaa. (Soma Waamuzi 7:2-7.) Wakati Gideoni alipochagua jeshi la watu mia tatu tu, Mungu alimwongoza kupata ushindi. Watu waliamini



kwamba Gideoni alikuwa mtu mkuu na walitaka kumfanya kuwa mfalme wao. Gideoni alikataa, na aliwaambia kwamba Bwana pekee ndiye aliyestahili kuwatawala.

SAMSONI:



Wakati Waebrania waliposhindwa na Wafilisti, Mungu alimchagua Samsoni kuwaamua Waisraeli na kuwaongoza. Samsoni alikuwa na nguvu mno. Lakini wakati wa vita, Samsoni jpia alimtendea Mungu dhambi. Wafilisti walimkamata, wakamng'oa macho.



Wakati Wafilisti walipokuwa wakifanya sherehe yao ndani ya jumba kubwa Samsoni alikuwamo; Samsoni alimwomba Mungu kumrudishia nguvu zake. Mungu alisikia maombi yake, na aliangusha jumba lile kubwa. Liliwaua Samsoni mwenyewe na Wafilisti wengi. Hapa tena Mungu aliwaokoa Waisraeli.

KAZI YA KUFANYA:

Waebrania walijua kwamba kulikuwa na Mungu mmoja tu lakini walianza kuabudu miungu wa uwongo walioitwa _____. Miungu hawa wa uongo walitengenezwa kwa _____, _____, _____, na _____. Mungu aliwaadhibu Waisraeli kwa kufuata miungu hawa wa uwongo.

Andika herufi "K" kando ya sentensi ya kweli, na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

- Mungu aliwaruhusu maadui za Waisraeli kuwashinda.
- Mungu aliwafanya Waebrania kuwa wagonjwa.
- Mungu aliwaruhusu Waebrania kuwa watumwa wa watu wale walioabudu sanamu.
- Mungu aliwaruhusu Wamisri kuwashinda Waebrania na kuwa-kamata, na kuwarudisha tena Misri.

Jaza nafasi zilizoachwa:

Wakati Waisraeli walipohuzunika na walipomlilia Mungu, Mungu aliwachagulia waamuzi _____ kuwaongoza. Watatu kati ya waamuzi hawa walikuwa _____, _____, na _____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Heri taifa ambalo Bwana ni Mungu wao, watu waliowachagua kuwa urithi wake." Zaburi 33:12

Wakati Waisraeli walipomwacha Mungu, hawakuwa chini ya ulinzi wake. Mungu aliruhusu mataifa maovu kuwashinda. Kila wakati walipomwacha Mungu, Mungu aliwafanya kuteseka. Mungu alikuwa akijaribu kuwafundisha Waisraeli ya kwamba yeye pekee ndiye aliyekuwa msaada na ulinzi wao.

Sisi sote tuna wajibu kwa Mungu kwa mambo tunayofanya. Kama tukifanya mambo mabaya, basi tunamwacha Mungu. Tutakuwa na huzuni. Mungu atatufanya kuwa na huzuni ili tujifunze kumwamini yeye. Inatupasa kila siku kukumbuka kwamba kuna Mungu mmoja tu, na kwamba Mungu huyo anatupenda na anatutunza.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Kumi na Moja

BAADHI YA WAEBRANIA WAFALME

MASOMO YA BIBLIA: 1 Samweli 10:1, 17-25; 1 Samweli 15:1-31; 16:1-13; 2 Samweli 5:1-5; 1 Wafalme 3:4-15; 1 Wafalme 8:22-30, 33-53, 55-61

Samweli ndiye aliyekuwa mwamuzi wa mwisho wa Israeli, lakini hakuwa kiongozi wa vita. Alikuwa kama nabii. Aliishi maisha yaliyompendeza Mungu nyakati zote. Hata wakati alipokuwa mdogo, Mungu alisema naye.

Wakati Samweli alipokuwa mdogo, alipelekwa na mamaye kukaa na kuhani Eli hekaluni. Wana wa kuhani Eli walitenda dhambi, wakawa waovu sana wakati Eli alipozidi kuwa mzee. Mungu hakutaka wana hao wa Eli kuwa makuhani wa Israeli. Alimwambia Samweli ya kwamba wana hao wanguuwa vitani wakati wa kupigana na Wafilisti.

Katika vita vilivyokuwa kati ya Wafilisti na Waisraeli, Wafilisti waliwaua wana wa Eli kama Mungu alivyosema, wakashinda Waisraeli. Waisraeli walijua kweli ya kwamba walikuwa wakiadhibiwa wakati huu

ambapo sanduku la Agano lilipotwaliwa na Wafilisti kutoka kwao.

Ilionekana kama kwamba Wafilisti walipata ushindi, na kwamba Bwana aliwaacha Waisraeli. Lakini Mungu aliwapiga Wafilisti kwa misiba iliyowafanya kurudisha sanduku la Agano kwa Waisraeli bila vita.

Wakati kuhani Eli aliposikia juu ya vifo vya wanawe, yeye pia alikufa, Samweli akawa kiongozi wa Mungu mahali pake. Samweli aliwaomba Waisraeli kumrudia Mungu na kusahau miungu wa watu wasio na dini. Aliwafundisha vijana na aliendelea kuwaambia mambo Mungu aliyo-mwambia. Wafilisti hawakushinda Waisraeli wakati huu, lakini Waisraeli walikuwa hatarini sikuzote.

Waisraeli hawakuridhika chini ya uongozi wa Samweli. Walitaka mfalme ambaye angetawala kama majirani zao wasio na dini walivyokuwa na mfalme. Samweli aliwaonya kwamba haikuwapasa kuwa na mfalme, akawaambia kwamba Mungu ndiye

aliyekuwa mfalme wao. Lakini watu hawakumsikiliza Samweli.

Samweli alimwomba Mungu, kisha Mungu alimwambia kumchagua Sauli mwana wa Kishi kuwa mfalme wa kwanza wa Israeli. Kwanza, Sauli aliwatumikia Mungu na Waisraeli vyema sana. Alimsikiliza Samweli wakati Mungu alipotaka kumwambia jambo la kufanya. Samweli alimfundisha Sauli jinsi ya kutawala vyema.

Sauli aliwaongoza Waisraeli kwa ushujaa sana wakati walipokuwa wakipigana vita na Wafilisti na Waamoni. Watu wa makabila yote ya Israeli walimfuata Sauli kama taifa moja. Walikuwa na nguvu nyingi na walimfuata Mungu.

Baada ya muda, Sauli alianza kupenda uwezo ambao Mungu alimpa. Choyo yake ilikuwa kubwa zaidi kuliko upendo wake kwa Mungu. Alifikiri moyoni mwake ya kwamba watu aliwatawala hawakuwa na thamani kama mambo yake ya anasa na utajiri.

Wakati Daudi alipomwua Goliathi, jitu la Wafilisti, Sauli alimwonea wivu sana hata alijaribu kumwua. Fikiria zake zilikuwa mbaya sana hata marafiki na jamaa zake waliogopa kumsogea karibu.

Mara nyingi Sauli hakumtii Mungu, na Mungu alisema ya kwamba hangekuwa mfalme tena. Ingawa Sauli alijaribu mara nyingi kumwua Daudi, Mungu alimlinda Daudi na alimfanya kuwa mfalme wa pili wa Israeli.



Daudi alikuwa tu kijana mchungaji wakati Samweli aliposema kwamba

angekuwa mfalme. Baadaye, Daudi alimpigia mfalme Sauli kinube chake kumfurahisha. Alijulikana sana na watu wakati alipomwua Goliathi. Alikuwa rafiki mpendwa wa Yonathani mwana wa Sauli. Daudi alikimbia kujificha kutoka machoni pa sauli ili kuokoa maisha yake. Ni mara mbili ambapo Daudi angalimwua Sauli kama angalitaka, lakini hakufanya hivyo. Sauli alipokufa Daudi alifanywa kuwa mfalme mahali pake.

Daudi aliwaongoza Waebrania kupata ushindi juu ya maadui zao. Alitawala vyema. Hakumpendeza Mungu sikuzote, lakini aliitwa mtu wa Mungu. Israeli ilikuwa nchi yenye nguvu sana chini ya utawala wa Daudi.



Daudi alifanya matayarisho kwa Sulemani kutawala mahali pake badala ya yeye kufa. Alijua kwamba Mungu alikwisha kumchagua Sulemani kuwa mfalme. Alimwonya Sulemani ya kwamba kama alitaka kufanikiwa, ilimpasa kuwa na nguvu na kufuata sheria ya Mungu.

Muda mfupi baada ya Sulemani kuwa mfalme, Mungu aliahidi kumpa kipawa cho chote ambacho angetaka. Sulemani alikuwa mwangalifu sana kumwomba Mungu kipawa kikuu ambacho angehitaji. Alimwomba hekima. Mungu alimtimizia ombi lake, naye (Sulemani) anajulikana sana kama mmojawapo wa wafalme wa Israeli waliokuwa na hekima nyingi.

Mungu alimruhusu Sulemani kujenga hekalu zuri Yerusalemu. Hekalu hilo lilikuwa mahali ambapo watu wangekusanyika kumwabudia Mungu mmoja wa kweli.

Sulemani alikuwa mfalme mwema wakati alipotenda mambo ambayo Bwana alimwamuru, lakini alianza kufanya mambo mengine pia. Alijivuna na alikuwa na choyo. Aliwashurutisha watu kulipa ushuru wa juu sana ili angeweza kununua vitu vya thamani nyingi. Alioa wanawake wengi wasio na dini, hata alifuata desturi nyingine zao. Aliacha kumwomba Mungu kumshauri na Waisraeli waligawanyika wakarudia tena kuabudu sanamu. Walihitaji tena ukombozi wa Mungu.

KAZI YA KUFANYA:

Andika herufi "K" kando ya sentensi ya kweli na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.


- Samweli alikwenda kukaa hekaluni wakati alipokuwa mdogo.
- Wana wa kuhani Eli wakawa makuhani wema.
- Wana wa kuhani Eli walikufa walipokuwa wakipigana vita na Wafilisti.

- Wafilisti hawakushinda Israeli wakati Samweli alipokuwa mwamuzi.
- Uchoyo wa Sauli ulikuwa mkubwa zaidi kuliko upendo wake kwa Mungu.
- Daudi alijaribu mara mbili kumwua Sauli.
- Wakati Daudi alipomwua Goliathi, Sauli alianza kumpe-na.
- Sulemani alichagua hekima kama kipawa kikuu alichohitaji kutoka kwa Mungu.

Andika maneno yafuatayo vizuri kukamilisha kila sentensi.

1. _____ (Swmeail) alikwenda kukaa hekaluni wakati alipokuwa mdogo.
2. _____ (Eil) alikuwa kuhani hekaluni.
3. _____ (Suila) alikuwa mfalme wa kwanza wa Israeli.
4. _____ (Diuda) alikuwa mfalme wa pili wa Israeli.
5. Daudi alimwua _____ (Galiothi), jitu la Wafilisti.

Chora duara kuzunguka kila picha inayokamilisha sentensi hizi.

Daudi ali-chunga	
Daudi alipiga	
Daudi alijificha katika	
Daudi alikuwa na	

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Bwana ndiye mfalme milele na milele; mataifa wamepotea kutoka nchi yake.” Zaburi 10:16

Labda inaweza kuonekana kwamba Waebrania hawakuwa wepesi kujifunza kumwamini Mungu. Walimwacha Mungu mara nyingi, lakini walikuwa wakijifunza. Mungu aliwasaidia Waebrania kupata watu wema kuwa wafalme wao. Mungu aliwafundisha wafalme hao jinsi ya kutawala. Kila mfalme alionekana kuwa mwema kuliko yule aliyemtangulia. Waebrania walikuwa wakijifunza kuwa watu wa Mungu.

Ni jambo baya sana kama mtu hapendi kujifunza. Tunapotenda kosa, tunajifunza kuepuka kutenda kosa hilo siku zijazo. Pia, tunafundishwa na Mungu. Mungu hataki tufanye dhambi na kufanya mambo mabaya. Lakini anajua kwamba tutafanya hivyo siku nyingine. Kwa hivyo, anataka tujifunze kutokana na kila dhambi tunayotenda ili tuweze kutenda mema.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Kumi na Mbili

WATUMWA KATIKA NCHI YA KIGENI

MASOMO YA BIBLIA: 2 Wafalme 17:5-18; 18:9-12; 24:1-20

Baada ya Sulemani kufa, Rehoboamu mwanawe ndiye aliyefanywa kuwa mfalme mahali pake. Watu walitumaini kwamba pengine angepunguza ushuru wao, na kufanya maisha yao kuwa rahisi, lakini hakufanya hivyo. Aliwazidishia taabu zao. Makabila kumi ya kaskazini waliasi, wakaanzisha ufalme mpya, wakamfanya Yeroboamu kuwa mfalme wao.

Rehoboamu aliendelea kuwa mfalme wa makabila mawili ya kusini. Makabila yale kumi yaliitwa Israeli, na makabila yale mawili yaliitwa Yuda. Watu wa Yuda waliitwa Wayahudi na mpaka sasa bado wanaitwa kwa jina hilo.

Yeroboamu aliwaongoza watu wake kumwacha Mungu. Alijenga mahali pengi pa kuabudia sanamu na hakuwaruhusu watu wake kwenda Yerusalemu upande wa kusini, kumwabudu Mungu. Makuhani wengi

na Walawi walihama Israeli kwenda kukaa katika nchi ya Yuda karibu na hekalu. Jambo hili lilifanya nchi ya Yuda kuwa na nguvu nyingi.

Rehoboamu alipotajirika na kuwa na nguvu nyingi, yeye pia aliwaongoza watu wake mbali na Mungu. Alijenga mahali pa kuabudia sanamu.

Waebrania waligawanyika katika falme mbili kwa muda ulio karibu miaka mia mbili. Walikuwa na wafalme wengi na wengi wao hawakumfuata Mungu. Kulikuwa na wafalme wachache tu waliokuwa wema katika wakati huu wa historia ya Waebrania.

Katika falme hizo mbili, kulikuwa na watu waliomjua Mungu na waliompanda. Baadhi ya watu hawa waliitwa na Mungu kuwa manabii na kuwaambia watu ujumbe wa Mungu. Wakati mwingine watu walimsikiliza Mungu, lakini kwa kawaida hawakufanya hivyo.

Manabii wengine waliteswa kwa sababu walisema ukweli. Maonyo ya



Mungu, sikuzote hayakuwa ya kupendeza kwa watu. Eliya, Elisha, Isaya, Yeremia, Hosea, na Amosi walikuwa wachache kati ya manabii waliokuwa muhimu sana.

Manabii waliwaambia watu juu ya upendo wa Mungu kwao, lakini walionya kwamba Mungu ange-waadhibu watu waliokataa kumtii. Walionya kwamba taifa la Waebrania lingegangamizwa kama watu

hawangerudia kumwabudu Mungu. Lakini watu hawakusikiliza manabii hawa.

Hatimaye Mungu aliwaruhusu jeshi la Ashuru kuishinda Israeli. Waisraeli walikamatwa mateka na walilazimishwa kufanya kazi kama watumwa katika nchi ya Ashuru.

Ufalme wa Yuda uliendelea kwa muda mrefu, lakini nao ulikuwa ukisahau Sheria za Mungu. Yeremia aliwaonya watu, lakini hawakum-sikiliza. Walimkamata, wakamfunga gerezani, wakatisha kumwua.

Kisha Mungu alimruhusu mfalme wa Babeli kushinda nchi ya Yuda. Watu wa Yuda walifanywa kuwa watumwa wa Wababeli. Utajiri wote wa Yuda ulitwaliwa ukapelekwa Babeli. Hekalu la Mungu liliteketezwa.

Mungu hakuruhusu watu wake wote kutawanywa. Hakutaka kutotimiza ahadi yake. Alikuwa akipanga kutumia watu wa Yuda kubariki ulimwengu kama alivyokwisha kuahidi.

Watu wa Yuda walikaa Babeli na hawakuteswa. Sasa walitaka kurudi kwa nchi yao ambayo Mungu aliwapa. Walikubali sasa kusikia ujumbe wa Yeremia.

Yeremia alikuwa na ujumbe mpya kwa watu. Aliwaambia kufurahi kwa sababu Mungu angeagana nao agano jipya. Aliwaambia pia ya kwamba Mungu alikuwa bado kusahau ahadi yake. Mungu angewatumia, na siku moja wangerejea katika nchi yao wenyewe.



KAZI YA KUFANYA:

Andika herufi "K" kando ya sentensi ya kweli na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

- Wakati Waebrania walipogawanyika katika falme mbili, walianza kumfuata Mungu.
- Yeroboamu na Rehoboamu waliwaongoza watu wao mbali na Mungu.
- Mungu aliwatuma manabii kama Eliya, Isaya, na Yeremia kuwonya watu ya kwamba Mungu angewaadhibu.
- Watu waliwasikiliza manabii wakaacha tabia yao ya kuto-mfuata Mungu.
- Mungu aliruhusu jeshi la Ashuru kushinda Israeli.
- Mungu aliwapeleka watu wa Yuda Babeli kama watumwa.

— Mungu aliacha kuwapenda watu wa Israeli kwa hivyo, alisahau ahadi yake kwao.

Chora mviringo kwa maneno ya kweli.

1. Baada ya Sulemani kufa, (Rehoboamu, Daudi) alifanywa kuwa mfalme.
2. Rehoboamu alikuwa mfalme wa makabila (mawili, matatu).
3. Yeroboamu aliwaongoza watu wake (kumfuata, kumwacha) Mungu.
4. Mungu aliwatuma (askari, manabii) kusema na watu wake.
5. Manabii wengi (waliteswa, wali-shukuriwa).

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Ee Mungu wa wokovu wetu, utusaidie, kwa ajili ya utukufu wa jina lako." Zaburi 79:9

Waebrania waliteseka sana kwa ajili ya dhambi zao. Wakati wote walipokosa kumtii Mungu na kufuata njia yao wenyewe waliadhibiwa. Mungu alikuwa bado akiwapenda watu hawa wake. Adhabu hiyo ilikuwa kwa ajili ya wema wa watu. Ilitolewa kuwarudisha watu wa Mungu kwake na kuwapa maisha ya furaha.

Wakati tunapotenda jambo baya nyumbani au shuleni, tunapoteza furaha yetu. Hatutaki kuwaona wazazi wetu au mwalimu wetu. Lakini baada ya kuadhibiwa, hatuwaogopi tena wazazi wetu na mwalimu wetu. Tunajisikia vizuri tena.

Mungu anataka tuungame dhambi zetu kwake. Ikiwa hatujakubali dhambi zetu kwa Mungu, tunamwogopa. Baada ya yeye kutasamehe, tunakuwa na furaha tena. Kisha tunaweza kusema naye tena katika maombi. Kwa hivyo, Mungu hutuadhibu wakati mwingine kuturudisha kwake na kutufanya kuwa na furaha tena.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA PILI KITABU CHA TATU

HISTORIA YA WAEBRANIA

© Copyright 1986, Baptist Publications House, All rights reserved.

J2 - 3Ps

Sura ya Kumi na Tatu

WAEBRANIA WARUDI TENA KWAO KANAANI

MASOMO YA BIBLIA: Ezra 1:7; 8:21-36; Nehemia 2:1-8; 6:15, 16; 8:1-9, 17, 18

Zaidi ya miaka hamsini iliyopita wakati Waebrania walipokaa kama mateka katika nchi ya Babeli. Walitendewa mema, lakini walitaka kurudi kwao. Waliomba mara kwa mara ili Mungu angewaruhusu kurudi Kanaani katika mji wao wa Yerusalemu waliopenda sana.

Baadaye, Koreshi mfalme wa Uajemi, alimshinda Nebukadreza mfalme wa Babeli. Alitawala Babeli pamoja na nchi ya Israeli. Koreshi alikuwa rafiki ya Waebrania ambao kwa kawaida waliitwa Wayahudi. Mungu alimsaidia kutenda haki kisha alianza kuwaruhusu Wayahudi kurudi Israeli.


Kundi la kwanza la Wayahudi waliorudi Israeli liliongozwa na Zarubabeli. Zerubabeli alikuwa kiongozi aliyechaguliwa na Mungu kuwaongoza Wayahudi kuanza kujenga tena hekalu la Yerusalemu. Walifurahi sana wakati msingi wa

hekalu jipya ulipokamilishwa, lakini watu wengine walikumbuka hekalu la zamani ambalo lilikuwa zuri sana.

Wayahudi walifanya kazi nyingi sana kulijenga hekalu lao, lakini hatimaye Koreshi rafiki yao alikufa. Mfalme aliyetawala mahali pa Koreshi alikataa kuruhusu ujenzi wa hekalu lile kukamilishwa, na kazi zote zilisimamishwa.

Lakini haikuchukua muda mrefu kabla mfalme mwingine kuchukua utawala. Alitambua kwamba Koreshi alipendelea ujenzi wa hekalu lile kukamilishwa, kwa hivyo aliruhusu ujenzi kuendelea. Baada ya muda mfupi Wayahudi walimaliza kujenga hekalu, wakamtolea Mungu sadaka ya kutekeza kama shukrani yao. Ilichukua miaka kama ishirini hivi kujenga hekalu lile jipya.

Wakati hekalu lile lilipokwisha kujengwa, Wayahudi walihitaji kiongozi mpya. Walihitaji kujifunza juu ya sheria ya Mungu. Mungu alimtuma Ezra ambaye alikuwa mwalimu na



mwandishi. Ezra alikuja na kundi lingine kubwa la Wayahudi waliokuwa wakirudi Israeli. Ezra alionyesha imani yake katika Mungu kwa kurudi bila askari au silaha za kujilinda.

Muda mfupi baada ya wao kurudi Yerusalemu, kundi hili jipya la Wayahudi walimtolea Mungu sadaka za kuteketezwa na shukrani katika hekalu lile jipya. Kisha Ezra alianza kusikia habari kuhusu dhambi za Wayahudi waliokuwa katika Israeli. Wayahudi hao walisahau sheria ya Mungu na walikuwa wakijiunga na majirani zao katika kutenda maovu.


Ezra alianza kufundisha, Wayahudi hao wakamsikiliza. Waliahidi kurudia ibada ya Mungu wa kweli.

Wayahudi walikuwa wamerudi Yerusalemu katika Israeli, lakini walikuwa na shida nyingi. Ezra alikuwa akiwafundisha sheria ya Mungu, lakini maadui zao waliwatisha. Kuta za mji wa Yerusalemu zilizokuwa na nguvu

zilikwisha kuharibiwa, na nguzo za mawe ndizo, zilizobaki zikisimama. Wayahudi walihitaji kiongozi ambaye angewaongoza kujenga tena kuta za mji kuwalinda. Mungu alimtuma Nehemia kwao.

Ingawa siku moja maadui wa Nehemia walimsimamisha njiani, aliweza kufika Yerusalemu. Mungu alimwambia ya kwamba kuta za mji wa Yerusalemu zilipasa kujengwa kuwazuia maadui za Wayahudi. Watu walisikia maneno ya Nehemia na walifurahi sana. Walianza kujenga.

Maadui hawakupendezwa walipoona kwamba mji wa Yerusalemu ungekuwa wenye nguvu tena. Walijaribu kusimamisha ujenzi. Lakini Wayahudi walifanya kazi usiku na mchana kujenga kuta za mji. Katika muda wa siku hamsini na mbili, kuta na milango zilikamilishwa.



Kwa furaha kubwa, watu walikusanyika katika Lango la mji, wakamwambia Ezra kuwasomea sheria ya Mungu. Walipokwisha kusikia

mafunzo yake, walilia machozi kwa sababu hawakufuata sheria hiyo. Waliahidi kuendelea kumwabudu Mungu na kuwafundisha watoto wao sheria hiyo katika miaka yote.

Historia ya Waebrania katika Agano la Kale inamalizikia kwa ahadi hii.

KAZI YA KUFANYA:

Chora mistari hadi kwa maneno ya kweli ya kumalizia kuonyesha mambo ambayo Mungu alimsaidia mfalme Koreshi wa Uajemi kuwafanyia Wayahudi.

Mfalme	kuchukua sehemu
Koreshi ali-	nzuri sana katika
waruhusu	Babeli.
Wayahudi	kurudi kwao Israeli.
	kujenga tena hekalu
	katika Yerusalemu.

Andika majina ya watu wanaotajwa habari zao katika sentensi zifuatazo:

Kiongozi aliyeanzisha kazi ya kujenga tena hekalu alikuwa _____.

Kiongozi aliyefundisha sheria za Mungu alikuwa _____.

Kiongozi aliyesaidia kujenga tena kuta za mji wa Yerusalemu alikuwa _____.

Wayahudi walipokwisha kurudi Israeli katika mji wao wa Yerusalemu, waliahidi kufanya mambo mawili. Tafuta mambo haya katika somo lako.

1. _____

2. _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie Bwana, naye ata-mrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atasamehe kabisa.” Isaya 55:7

Wayahudi walijifunza somo muhimu sana katika Babeli. Mungu tu ndiye angeweza kuwalinda na kuwaongoza. Walipotaka kurudia uongozi wa Mungu, Mungu aliwatumia viongozi. Viongozi hawa Mungu aliwachagua kufanya kazi fulani. Mmoja angejenga hekalu, mwingine angefundisha sheria ya Mungu, na mwingine angejenga tena kuta za Yerusalemu.

Mungu ndiye anayetupa viongozi siku hizi. Tunapokataa kumtii Mungu, na tunapomwacha, tunapata viongozi wasiofaa kwa sababu ni sisi wenyewe ndio tunaowachagua bila msaada wake. Lakini tunapochagua kumtafuta Mungu, anatupa viongozi alio-wachagua yeye mwenyewe.

Tunahitaji kumshukuru Mungu kila siku kwa sababu amekwisha kusema na watu wake aliowachagua. Amekwisha kuwaita watu wengi kuwa wachungaji na waalimu. Labda Mungu ana kazi maalum kwako kufanya siku moja.

